Msururu wa Upotofu na Udanganyifu

Uongozi wa Mtume
Toleo la (2)

# Zungumzeni na Watu Vizuri



SANAD

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila Jinsi ya sifa njema ni za Allah, Na Rehema na Amani zimshukie Mtukufu wa Manabii na Mitume, Bwana wetu Muhammad aliyetumilizwa ni rehema kwa viumbe, ziwashukie na jamaa zake na maswahaba zake wote. Amesema Allah aliyetukuka:

{Na tulipofunga agano na Wana wa Israili: "Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na simamisheni Swala, na toeni Zaka." Kisha mkageuka isipokuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuza.} [1]

## Umoja wa Maadili na Tabia

Tabia: ni hali iliyokita katika nafsi inatokamana nayo vitendo na maneno bila kufikiria na kujipanga.

Tabia njema ni sifa ya ubinadamu ambayo imelinganiwa na kila sheria ya kutoka mbinguni.

Tabia njema ni sifa inayofungamana na maumbile ya binadamu.

Maadili na sifa nzuri zimethubutu na wala hazikubali kujigawanya, kujifunga au ubaguzi.

Kama hali ni namna hii, basi kwa nini tunaandika makala hii?

Hakika katika yanayotukumba leo kuhusiana na kuporomoka katika tabia ni hatari kwa nidhamu ya tabia njema ambayo tumeelekezwa na sheria za mbinguni. Na ni kasoro ya kinafsi (nafsi ya mwanadamu), sababu umbile la mwanadamu halijui kubagua katika hukumu zake, ndipo ummah ukapatikana na upungufu wa kujua thamani ya maneno na vitendo vizuri, imma kwa mtu binafsi au kwa vipote. Yote hayo inatupelekea tukwame na kujibu maswali kadhaa yanayofungamana na aya iliyotangulia.

- Je wanaokusudiwa katika aya ni Wana wa Israili peke yao kama wanavyodai baadhi au inachanganya na umma huu pia?
- Na jee hii aya imefutwa kwa aya ya upanga (kupigana) au bado hii ipo?
- Katika hii aya, neno "watu" wanakusudiwa nani?
- Katika hii aya, inakusudiwa nini "kusema kwa wema"?
- Kuna mafungamano gani baina ya kuamrishwa kusema kwa wema na maamrisho yaliyokuja katika aya hio hio?

1- Surah al-Baqara:83

## Ni Nani Anaekusudiwa Katika Aya?

Muktadha wa aya unadhihirisha wazi wazi kuwa mafunzo yalioko katika aya tumeelekezewa sisi katika sheria ya kiislamu. Mwenyezi Mungu ametuamrisha kumpwekesha, kuwatendea wema wazazi, jamaa wa karibu, mayatima na maskini, na ametuamrisha kuswali na kutoa zaka. Na baina ya hayo mafunzo, imekuja amri ya kusema vizuri na kila mtu. Vipi itawezekana kuihusisha hii amri kuwa ni ya Wana wa Israili peke yao?

Haiingii akilini kuwa kuamrishwa kuwa na tabia njema iwe ni haswa kwa Wana wa Israili tu, na amri hii iwe haiko kwenye sheria ya uislamu ambayo ndiyo iliyohitimisha sheria zote. Kama ambavyo haifai kuzingatia kufutwa au kubadilishwa tabia njema na maadili, na ambazo ni katika maumbile yaliyosalimika, haswa kuwa Mtume ﷺ amesema, "Nimetumilizwa kutimiza tabia njema."[2]

Pamoja na haya, Imam al-Fakhr ar-Razi katika kitabu chake at-Tafsir al-Kabir na Imam Abu Hayyan al-Andalusi katika al-Bahr al-Muhit, wametaja dalili kutoka kwenye Qur`an zinazotilia mkazo kuwa hizi aya zimewaenea Ummati Muhammad kwa kuwataka wafuate haya mafunzo mazuri ya hali ya juu na kuwa yamebaki bila kufutwa. Walisema, "Amedai Abu Jafar Muhammad bin Ali al-Baqir kuwa hii kuenea imebaki vile vile kama ilivo dhahiri yake na kuwa hakuna haja kuifanya ni haswa --na kauli hii ndiyo yenye nguvu Zaidi. Na dalili yake[3] ni kuwa Musa na Harun --pamoja na utukufu wao-- wameamrishwa wafanye ulaini na upole kwa Firaun. Pia Mtume wetu Muhammad ameamrishwa kufanya upole na asifanye ugumu. Na Mungu aliposema {Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema} [4]. Na Mola aliposema {Wala msiwatukane hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua}[5]. Na aliposema {Na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa hishima yao}[6].
Na aliposema {Na wapuuze majahili}[7].

Ibn Ajibah amesema katika tafsiri yake, "Kila ahadi iliyochukuliwa kwa Wana wa Israili pia imechukuliwa kwa Ummati Muhammad. Na hii ndiyo hikma ya sisi kutajiwa visa vyao na kuelezwa makosa yao ili tujiepushe kuangukia waliyoangukia wao, tusije tukaangamia kama walivyo angamia."[8]

2- Musnad al-Bazzar 15/364. Na katika riwaya "Nimetumilizwa kutimiza tabia vizuri."
3-Tafsir ya ar-Razi na Tafsir al-Bahr al-Muhit ya ibn Hibban
4-Surah an-Nahl:125
5-Surah al-An'am:108
6-Surah al-Furqan:72
7-Surah al-A'araf:199
8-Tafsir ibn Ajiba

**Haiwezekani kuzingatia kuwa tabia na maadili zinaweza kufutwa ambapo ni katika maumbile ya kibinaadamu yaliyosalimika.**

Aghlabu ya waliofasiri Quran wamelemea kwenye kauli ya kuwa haya mafunzo yameenea Ummati Muhammad na kuwa yamebaki wala hayajafutwa, japokuwa wananukuu mapokezi ambayo yanasema kinyume na hivo.

Al-Alusi amesema katika tafsiri yake, “Na anaesema kuwa waliokusudiwa ni umma huu, na kuwa haijafutwa au anaesema kuwa imefutwa kwa aya ya upanga au (watu) wanaokusudiwa ni waumini wema pekee kwa kuwa hakuna kusema vizuri pamoja na makafiri na mafasiki kwa sababu tumeamrishwa tuwalaani na kuwatukana na kuwapiga vita, anaesema hivi ameenda mbali na usawa.” [9]

## Ni Nani Wanaokusudiwa kwa Neno "Watu" Kwenye Aya?

Aya tukufu imekuja kueleza ahadi ya jumla aloichukua Mungu kwa Wana wa Israili. Na imetangulia kuwa baadhi ya Wana wa Israili walikatazwa kufanya ubaguzi katika maadili mema. Wakawa wanatumia maadili mema wanapoamiliana na watu wao na wanakosa kutumia maadili mema wanapoamiliana na wasiokuwa wao. Mwenyezi Mungu ameeleza haya aliposema: {Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya mrundi wa mali atakurudishia. Na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipokuwa ukimsimamia kumdai. Haya ni kwa kuwa wakisema: “Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma.” Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua. Sivyo hivyo, bali anayetimiza ahadi yake na akamcha Mungu basi Mwenyezi Mungu huwapenda wacha Mungu.} [10]

Basi ni vipi itawezekana Mungu achukue ahadi kwao ambayo itakuwa na ubaguzi huu huu wa tabia na maadili ambao ameukataza?

Imekuwa wazi kuwa makusudio ya aya ni watu wote kwa jumla na kuwa misingi mema na maadili hayajui ubaguzi. Wanaosema kuwa amri ya Mola hapa (katika hii aya) inawaenea watu wote ni:

Imam Ali bin Abi Talib, Imam Muhammad al-Baqir bin Ali Zayn al-Abidin bin al-Husayn, Ataa bin Abi Rabah kama al-Hafidh as-Suyuti alivyowanukuu katika kitabu ad-Durr al-Manthur na ndiyo rai walioikubali Shekhe wa Mufassirina Ibn Jarir, Imam al-Fakhr ar-Razi, al-Hafidh Ibn Kathir, Imam Abu Hayyan al-Andalusi, Imam al-Qurtubi, Imam al-Mawardi, Imam as-Saawi, Imam al-Buruswi, Imam al-Biqa’i na Tahir bin Ashur katika tafsiri zao za Qurani Tukufu.

9-Tafsir Ruh al-Ma’ani ya al-Alusi
10- Surah Aal ‘Imran:75-76

Tuna haja sana kuzingatia maneno ya Imam al-Qurtubi alipotafsiri hii aya akasema, "Mtu anafaa awe ni mwenye maneno laini na uso wa bashasha kwa watu, sawa kwa mtu mwema au muovu, au mtu wa sunna au bid'a bila kudanganyana."[11]

Kwahio {Na semeni na watu kwa wema} inawaenea watu wote kwa jumla.

## Ni Yapi Makusudio ya Maneno Mazuri Katika Aya?

Ilivyo wazi katika aya na muktadha wake ni kuenea kila aina ya uzuri wa maneno kwa kadri inavyowezekana, bila kuhusisha aina maalum ya maneno kuliko kingine, kwa sababu yaliyotangulia yamehusisha aina maalum ya kuamiliana kwa vizuri ambayo inakusanya maneno na vitendo kama kuwatendea wema wazazi wawili na jamaa wa karibu na mayatima na maskini. Kwahio hailingani baada ya haya kuletwa jambo la jumla kwa kusudia jambo mahsusi. Zimepokewa riwaya kutoka kwa Abdullah bin Abbas zinazohusisha, pamoja na hivo al-Hafidh Ibn Kathir ametanabahisha katika tafsiri yake ya kuwa baadhi wanapofasiri maneno mazuri hapa kwa tafsiri mahsusi haiangushi maana ya ujumla bali inaingia chini yake. Akasema, "Yaani inamaanisha zungumza nao kwa vizuri na ulaini." Na inaingia katika tafsiri hii kuamrisha mema na kukataza maovu kama alivyosema Hasan al-Basri katika neno lake Allah aliyetukuka {na semeni na watu kwa wema}: Wema wa maneno ni kuamrisha mema na kukataza maovu na afanye upole na asamehe na aseme na watu kwa wema kama Allah alivosema, nayo ni kila tabia njema ambao Mungu anairidhia.
Na imepokewa maana ya aya kutoka kwa Imam Muhammad al-Baqir ambayo inafidisha kutilia mkazo mafungamano ya aya na uadilifu wa misingi, aliposema, "Zungumzeni nao kwa namna muayotaka wao wazungumze nanyi." [12]

Na walikuwa baadhi ya wema waliotangulia wakiwasalimia Watu wa Kitabu. Akalaumiwa kuhusu hilo akasema Mungu amesema {Na semeni na watu kwa wema}, nayo ni salamu.[13]

Kwahio {Na semeni na watu kwa wema} inaenea kila aina ya uzuri wa maneno na haijafungika katika aina maalumu ya maneno.

**al-Ahnaf bin Qays alisema, "Je nisiwaambie maradhi mabaya zaidi?" Wakamwambia, "Kwani." Akawaambia, "Ni tabia mbaya na ulimi mchafu."**

11-Surah al-Baqara:83 Tafsir al-Qurtubi
12-Tafsir Zad al-Masir ya Ibn al-Jawzi
13- Tafsir ibn Kathir

## Uzuri wa Dhahiri na wa Ndani

Kuyafanya maneno mazuri ndicho kiwango ambacho unaweza kuamiliana na watu wote. Kisha hapana budi huu uzuri wa maneno uwe unatoka kwenye moyo na sio kupamba kwa maneno tu. Kwani Muislamu anapowaambia watu maneno mazuri huwa amewatakia kheri na hio ndiyo asili ya uzuri wa kuamiliana na viumbe.[14] Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema, "Haamini mmoja wenu hadi ampendelee mwenzake kile anachojipendelea nafsi yake."[15] Na ilipokuwa mtu hawezi kuwafanyia watu wote wema kwa vitendo ndipo Allah akaamrisha {Na semeni na watu kwa wema}. Akiwa mtu atashindwa kusaidia watu wote kwa vitendo, basi asiwe bakhili wa kuamiliana nao vizuri na kuwaambia maneno mazuri na kuwapa nasaha.[16]


## Amri Hii Ina Mafungamano Gani na Maamrisho Mengine Katika Aya?

Zingatia nami ewe ndugu yangu kipenzi muktadha ya aya: {Na tulipofunga agano na Wana wa Israili: "Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na simamisheni Swala, na toeni Zaka." Kisha mkageuka isipokuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuza.} [17]

Aya imekusanya agano na ahadi iliyochukuliwa kwa Wana wa Israili ambalo limekusanya mambo mengi:

- Kumpwekesha Allah kwa kumuabudu.
- Kuwafanyia wema wa maneno na vitendo (wazazi, kisha jamaa, kisha mayatima, kisha maskini).
- Maneno mazuri kwa watu wote.
- Kusimamisha swala na kutoa zaka.

Kisha akawakosoa wengi wao kwa kutolazimiana kwao na ahadi




---

14-Tafsir at-Tahir bin 'Ashur
15- Sahih Bukhari, Mlango wa ni katika imani mtu kumpendelea mwenzake anachojipendelea nafsi yake, Sahih Muslim Mlango wa ni katika alama za imani mtu kumpendelea kheri muislamu mwenzake anachojipendelea nafsi yake.
16-Tafisr al-Biqa' i
17- Surah al-Baqara:83

Kwa namna mbali mbali, tunaona utukufu wa amri hii katika aya:

* Uelekezi wa Allah umekusanya baina kufanya wema wa maneno na vitendo.[18]
* Mungu ametanguliza kufanya wema wa maneno na vitendo kabla ya swala na zaka pamoja na kuwa hizi ni katika faradhi muhimu zaidi bali ni katika nguzo za uislamu! Basi itakuwa imeashiria kuwa kufanya wema ndiyo asli ya miamala yote ambayo tumeamrishwa na Mola aliyetukuka.

## Ufupi

Imebainika kuwa aya hii {Na semeni na watu kwa wema}:

- Inaenea kila mtu na haihusiki kwa wema au waumini pekeyao.
- Inakusanya maana za wema zote, na sio kuamrisha mema na kukataza maovu pekee.
- Imethubutu kwenye sheria ya kiislamu, na si haswa kwa Wana wa Israili.
- Inatumika na imebaki wala haijafutwa.

***Kila jeraha lina dawa***

***Tabia mbaya haina dawa***

***Ali bin Abi Talib (Mungu autukuze uso wake)***

(18) Tafsir ibn Kathir

# Msururu wa Upotofu na Udanganyifu

Mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie na jamaa zake) amesema, “Wataipokea hii elimu [Dini] waadilifu katika kila watakaokuja. Wataiondolea upotofu wa waliopotoka na uvamivizi wa wabatilishaji na upotoshaji wa wajinga.” [19]

Baadhi ya wenye fikra za makosa wamefahamu maneno ya Allah Mtakatifu na maneno ya Mtumi wake ⍰ kwa namna isiyoafikiana na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa wema waliotangulia wala haziendani na makusudio na misingi mikubwa mema ya Ujumbe wa Mungu.

Wakakusudia baadhi ya aya za Qur`ani Tukufu ambazo zilioteremka kwa ajili ya wasiokuwa waislamu wakazitumia kwa waislamu. Na wakatumia aya zilizokuja katika hali fulani wakazifanya ni za kutumiwa kila mahali. Na wakaharibu maana ya maneno ya Mungu na hadithi ya Mtume wake mtukufu kwa namna imepeleka kukita au kujengeka fahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kupatikane vitendo ambayo havina mafungamano na uislamu Dini ya Amani ya Kiislamu.

Tutajua kupitia msururu huu kuhusu upotoshaji uliopatikana katika maana za maneno ya Mungu na maneno ya Mtume wake waliouangukia wenye fikra hizi za makosa, na upotevu katika hukumu fulani, na kubeba fahamu za makosa ambazo zimewafanya wapambunakane na makusudio ya Mungu na Mtume wake na fahamu ya wema waliotangulia.

19- Hadithi mashhuri imesahihishwa na ibn Abdul Barr, na imepokewa kuwa Ahmad bin Hanbal amesema, “Ni hadithi sahihi.”

دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION

SANAD

www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork